



## ***Waustralia Wafrika: Ripoti juu ya haki za binadamu na masuala ya kujumuishwa kwa jamii – Muhtasari wa Karatasi ya Majadiliano***

### **Tunataka kujua unachofikiria**

Tunataka kusikia hadithi za makazi na haki za binadamu za Waustralia Wafrika katika Australia nzima.

Tunataka kusikia mawazo yako kuhusu mambo ambayo yanaweza kubadilishwa ili kufanya makao ya Australia kuwa rahisi.

Tutatumia mchango wako katika kukuza ripoti ya mwisho. Tunatumaini kwamba ripoti ya mwisho itashawishi watu na mashirika yanayofanya maamuzi na kutoa huduma, na kusaidia kubadili maoni ya Waustralia wengine kuhusu Jamii za Kiafrika.

### **Je, karatasi ya majadiliano hufanya nini?**

Hutoa maelezo na huwauliza Waustralia Wafrika (na mtu yeyote ambaye anayetaka) kutuambia juu ya hadithi, masuala na hoja zao.

### **Unaweza kusema nini?**

Maarifa na maoni yako yanaweza kutusaidia kukusanya haki za binadamu na masuala ya kujumuishwa kijamii kwa jamii za Waustralia Wafrika.

Tunataka haswa kusikia kutoka kwako kuhusu maarifa yako nchini Australia juu ya ajira na mafunzo; elimu; afya na maslahi; makao; na mifumo ya haki na sheria. Unaweza pia kutuambia masuala au hoja zingine zozote ambazo unazo.

### **Unawezaje kutuambia hadithi yako?**

- Njoo kwa mikutano na vikundi ambayo tutavipanga katika Australia (vingine vitakuwa na wafasiri ili kukusaidia kuhusika)
- Fanya uwasilisho kwa kutuandikia (angalia maelezo hapa chini)

### **Ni wapi unaweza kujua zaidi kuhusu mikutano?**

- Mitandao ya jamii itasakusaidia kupata maelezo
- Ratiba itakuwa kwenye tovuti yetu ya: [www.humanrights.gov.au/africanaus](http://www.humanrights.gov.au/africanaus) kuanzia tarehe 15 Machi 2009 (kwa Kiingereza)

## Ni nani anayetusaia?

**Mradi huu unaongozwa na kuungwa mkono na Kamati Elekezi na** Kikundi cha kitaifa cha Marejeo ya Jamii. Kamati Elekezi inamawakilishi wawili wa jamii: Samia Baho, Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Masuala ya Wanawake Waaustralia Wafrika na Abeselom Nega, Mwenyekiti Aliyetoka hivi karibuni wa Shirikisho la Baraza la Jamii za Kiafrika; na mwakilishi wa mtoa huduma Eugenia Tsoulis, Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Nyenzo za Uhamiaji cha Australia Kusini.

**Ushauri wa kitaifa utaratibiwa na chombo kinachoitwa Myriad Consultants.**

**Washirika wengine ni pamoja na:** Huduma za Elimu ya Watu wazima wa Jamii anuwai (AMES) katika Victoria; Msalaba Mwekundu wa Australia; Taasisi ya Afya Anuwai; na Idara ya Familia ya Serikali ya Australia. Huduma za Jamii na Mambo ya Asili (FaHCSIA).

### **Jinsi ya kulalamika**

Kama uwasilisho wako uko kwa Kiingereza tunapendekeza kwamba ututumie barua pepe kwa: [africanaus@humanrights.gov.au](mailto:africanaus@humanrights.gov.au)

Kama huwezi kututumia barua pepe, au ikiwa uwasilisho wako umeandikwa kwa lugha yako, tuandikie kwa:

*African Australians project* submission  
Race Discrimination Unit: Education and Partnerships Section  
Australian Human Rights Commission  
GPO Box 5218  
Sydney NSW 2001

au tuma na faksi kwa: (02) 9284 9849.

### **TAREHE YA MWISHO YA MAWASILISHO: 30 Juni 2009**

#### **Siri**

Mawasilisho yatahughulikiwa kama hati za umma isipokuwa utuambie kwamba unataka uwasilisho wako uwekwe siri. Tafadhali tuambie katika uwasilisho wako kwamba ni ya siri.

## Ninawezaje kupata maelezo zaidi?

- Kama Kiingereza sio lugha yako ya kwanza, waulize wengine katika jamii yako kusaidia au kujaribu mashirika ya jamii ambapo wafanyikazi wanaweza kusaidia
- Nenda kwa tovuti yetu [www.humanrights.gov.au/africanaus](http://www.humanrights.gov.au/africanaus)
- Tutumie maswali yako kwa barua pepe [africanaus@humanrights.gov.au](mailto:africanaus@humanrights.gov.au)
- Tupigie simu na maswali yako, nambari ya simu (02) 9284 9600 or 1800 620 241 (TTY)

## Unapitia ubaguzi?

Kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako chini ya sheria ya ubaguzi:

- Nenda kwa [www.humanrights.gov.au/complaints\\_information/index.html](http://www.humanrights.gov.au/complaints_information/index.html)

- Nenda kwa [www.humanrights.gov.au/about/languages/index.html](http://www.humanrights.gov.au/about/languages/index.html) (ikiwa hakuna karatasi ya maelezo katika lugha yako, tunaweza kupanga mkalimani ajadili malalamiko yako, kwa hivyo tupigie simu)
- Piga simu **kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu**, nambari ya simu 131 450, sema lugha yako na uulize Tume ya Haki za Binadamu ya Australia, nambari ya simu 1300 656 419
- piga simu kwa Laini ya Maelezo ya Malalamiko, nambari ya simu 1300 656 419